Ijue Biblia Yako

# UUNGU
## (GODHEAD)

**Mafunzo ya Biblia Ngazi ya Juu**

**Na,**

**J e r r y  B a t e s**

# Uungu

Toleo la II, 2021

Tafsiri

(Translation)

**Peter Kamatula**

Mhariri

(Proof reading)

**John B. Haule**

Mpangilio

(Layout)

**Shadrack S. Msambaza**

Nakala kwa lugha ya Kiswahili na,

**Swahili Gospel Team (SGT)**
**swahiligospelteam@gmail.com**
**Arusha, Tanzania**

# Utangulizi

Mwandishi wa kitabu hiki ndugu Jerry Bates, ni mhubiri na mwalimu mwenye uzoefu wa muda mrefu katika masomo ya Biblia. Pia amebobea katika uchambuzi na uandishi wa vitabu, ameandika vitabu mbali mbali vya kidini. Kama ilivyo katika vitabu vingine, katika kitabu hiki ameonesha umahiri wake wa ufundishaji kwa njia ya uandishi na kuhakikisha kila anayebahatika kusoma kitabu hiki anaelewa vizuri kuhusu ujumbe ambao Biblia inamzawadia kila mtu kwa upendo wa dhati utokao kwa Mungu wetu.

Kitabu hiki ni fursa adhimu ya kujifunza kuhusu Uungu. Ingawa somo hili ni gumu, lakini mwandishi ametumia mbinu rahisi zinazoweza kumfanya mtu kuelewa vizuri kuhusu Uungu.

Kila mwisho wa mada kuna kipengele cha maswali ambacho ni mahususi kwa wewe kujipima katika kile ulichojifunza.

Tunapendekeza kitabu hiki kisomwe na kila mtu kama sehemu ya kujifunza Maandiko Matakatifu na kupata fursa ya kutenda kwa usahihi mapenzi ya Mungu.

Tunakushukuru kwa kutenga muda wako ili usome kitabu hiki! Ni matumaini yetu utawashirikisha na wengine ujumbe utakaojifunza katika kitabu hiki.

“Amani na upendo wa Bwana wetu Yesu Kristo, katika ushirika wa Mungu Baba na Roho Mtakatifu uwe nawe daima!”

**Swahili Gospel Team (SGT)**
swahiligospelteam@gmail.com
**Arusha, Tanzania**

# Yaliyomo


1. Umuhimu wa Uungu 1
2. Yesu ni Mungu 13
3. Roho Mtakatifu ni Mungu 25
4. Bwana Mungu wetu ni mmoja 35
5. Nini maana ya Nafsi Tatu katika umoja? 43

# 1

## UMUHIMU WA UUNGU

Somo la Uungu “ni moja ya mafundisho ya ukristo yanayopingwa na kijadiliwa sana, lakini pia bado ni moja ya mambo ya msingi. Haipaswi kushangaza kwamba tunaona ni vigumu kumwelewa Mungu kwa sababu tunataka tumwelewe Mungu asiye na ukomo kwa akili zetu zenye ukomo. Hata hivyo, ni muhimu kwamba wakristo wawe na uelewa wa fundisho hili muhimu. Fundisho la “Uungu” lina maana kwamba wote watatu, Mungu Baba, Yesu Mwana na Roho Mtakatifu ni Mungu, lakini sio miungu watatu, bali ni mmoja.”Uungu” limetokana na neno la Kilatini lenye maana “watatu katika umoja”; kwa hiyo, Uungu hurejelea “hali ya utatu katika umoja” wa Mungu. Kwa kuwa hili ni gumu kulielewa, wengi hulipinga wazi wazi, au wanalibadilisha kwa namna fulani ambayo hupelekea kuukana Uungu kamili wa Yesu au Roho Mtakatifu au wote wawili. Katika mfululuzo huu wa masomo, kwanza tutaliangalia swali, “Je, fundisho la Uungu linaleta tofauti yoyote?” Halafu tutaangalia ushahidi wa kibiblia wa Uungu wa Yesu na Roho Mtakatifu. Mwisho tutajifunza juu ya swali, “Je, fundisho la Uungu linaleta maana yoyote?”

## Kwa nini wengine wanatafuta kuliacha fundisho hili?

Wengine wangesema kwamba kwa kweli fundisho huleta tofauti ndogo. Katika mtazamo wao, hakuna hoja ya muhimu ya kimaadili au iliyonyoofu ambayo ingebadilishwa, hata kama Uungu haukuwa wa kweli. Sehemu kubwa ya fasihi ya kikristo ingebadilishwa kidogo sana. Kihalisia, wakristo wengi kwa kweli hawaelewi fundisho la Uungu, kwa hiyo hii inaleta tofauti gani?. Kipimo ambacho wengi wanakitumia kuuhukumu ukweli ni, “Hili linanisaidia nini?” kwa maneno mengine ni kwamba, kama halinisaidii kufikia malengo na shauku yangu, basi linapaswa litupiliwe mbali na kupuuzwa. Fundisho hili pia hugawa (huleta mgawanyiko), kwa hiyo, kwa mujibu wa baadhi ya wakristo linapaswa kuachwa. Kwa wengine ni kikwazo kikubwa cha Imani katika Yesu. Kutokana na sababu zilizotolewa hapo juu, wengi wanasema kwamba Uungu huleta tofauti ndogo kihalisia kwa mkristo na kwa hiyo kiuhusiano si muhimu.

Kwa namna fulani, mmomonyoko wa imani katika Uungu, unawakilisha maelezo mapya ya maana ya ukristo kwa jumla. Kinachosisitizwa mara nyingi katika dini za leo ni hisia au mvuto wa dini juu ya hali ya kijamii tunazoishi. Katika hali yoyote ile, Uungu hauendani na hali hizo, kwa hiyo, kwa mara nyingine tena, wengi wanasisitiza kwamba fundisho hilo liachwe.

Fundisho la Uungu pia ni chanzo kikubwa cha upinzani na mzaha kwa dini nyingine. Dini nyingine mara nyingi zinaushutumu ukristo kuwa na imani ya miungu wengi, kwa sababu tunaaamini Uungu, ambao katika mawazo yao humaanisha miungu watatu. Kizuri zaidi, fundisho hili linafumba (linahitaji kufumbuliwa); kibaya zaidi linaonekana kama mkanganyo ulio dhahiri. kwa kuwa Uungu ni chanzo kikubwa cha upinzani, tena wengi wangependa kuachana na fundisho hili linaloleta mgawanyiko.

## Umuhimu wa utatu wa Mungu

Hata hivyo, fundisho hili si dogo au la pembeni, kwa sababu linahusisha asili ya Mungu alivyo. Jambo moja katika Uungu linalosumbua ni "Mungu kuvaa mwili" au "Mungu kufanyika mtu". Mara nyingi mtu hufikiria Mungu huwa wapi wakati shida na majanga yanatokea? Hali ya Mungu kuwa katika mwili inatueleza kwamba si kwamba Mungu hajali matatizo ya ulimwengu; lah, bali alifanyika kuwa sehemu ya ulimwengu ili auokoe. Fundisho hili pia linaondoa wazo lisilokuwa la mpango wa kimaadili wa sehemu ya tatu isiyo na hatia kuadhibiwa. Kama Yesu ni sehemu ya Uungu, basi hakuwa mwathirika asiyehiari kufa (alihiari).

Zaidi ya hapo, Uungu unatofautisha ukristo na dini zingine. Katika jamii yetu yenye wingi wa dini, dini zote zinatazamwa kimsingi kama ziko sawa, na tofauti zilizopo kati ya dini hizi zinaweza na zinapaswa kupatanishwa au kupuuzwa. Walakini Uungu hufanya imani ya jinsi hiyo isiwezekane. Uungu hauwezi kuchanganywa na dini nyingine, ni wa kipekee.

Swali la, "tupeleke sala zetu kwa nani?" Linajadiliwa sana miongoni mwa wakristo. Kwa kuwa Biblia haijawahi kutuamuru kumwomba yeyote isipokuwa Mungu Baba, basi sala zote zielekezwe kwa Mungu Baba tu. Namna hii ya kumwendea Mungu kwa sala inaonesha kazi ya kila nafsi katika Uungu kama nafsi kamili inayojitosheleza. Walakini kimsingi wazo la Uungu linaonesha kwamba wakati kazi fulani zinatakiwa kufanywa na mshirika mmoja wa Uungu huo; lakini nafsi zote zinashirikishwa katika mambo yote. Roho Mtakatifu husaidia katika maombi yetu kwa Mungu, katika jina la Kristo (Rum.8;26-27. Yn.15;16:23). Hivyo, wakati tunapomuomba Mungu Baba, wote wanajumuishwa katika kuijibu sala, na hili linatulazimu tuulize swali juu ya mgawanyiko mkuu kama huo katika kazi ya washirika tofauti tofauti wa Uungu. Sala zetu na ibada zetu zinaelekezwa katika Utatu wa Mungu badala ya Mungu Baba tu.

## Namna tunavyohusiana sisi kwa sisi utegemea Uungu?

Uungu unakuwa kielelezo kwetu namna tunavyopaswa kuhusiana kila mmoja na mwenzake. Washirika wote watatu wa Uungu wako sawa milele. Tutajadili baadhi ya vifungu vya maandiko vinavyoonesha utii wa Yesu katika somo lingine, lakini inatosha kusema kwamba utii wote wa Yesu uchukuliwe kwamba ni sehemu ya hali yake ya kuvaa mwili duniani na wala si asili yake ya milele. Yesu alisema kwamba tunatakiwa kuwa na umoja, kama vile Yeye na Baba walivyokuwa na umoja (Yohana 17;11,21). Kwa hiyo uelewa wa umoja wa Uungu ni lazima ili tuelewe hakika namna sisi kama wanafunzi wake tunavyopaswa kuwa wamoja.

Jambo la kwanza, wakristo wote wanapaswa kuchukuliana kuwa sawa katika thamani. Wakati kiukweli wengi wana karama, uwezo na kazi tofauti tofauti; hata hivyo sisi ni wamoja katika thamani mbele za Mungu. **Hakuna Myahudi wala Myunani, hakuna mtumwa wala huru, hakuna mtu mume wala mtu mke maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu** (Wagalatia 3: 27-28). Hivyo, kwa hali yoyote mshirika mmoja akimtawala mwingine, au mtu kuhesabiwa kama mwenye thamani ndogo, hiyo haifai. Matatizo mengi yamejitokeza ndani ya kanisa pale ambapo mtu mmoja au kundi la watu halijali mahitaji,

hali au shauku ya wengine, na mapambano ya mamlaka yamejitokeza. Nafsi moja (kati ya nafsi za Uungu) haiwezi kuwa na hali ya kupambania mamlaka katika Uungu; kwa sababu hiyo, hali kama hiyo haipaswi kujitokeza katika kanisa pia.

Jambo la pili, asiwepo mtu wa kuinuliwa juu ya mwingine. Ni dhahiri, washirika wengine kama vile mhubiri au viongozi wa kusanyiko wana majukumu yanayoonekana wazi kuliko wengine. Wengine wana karama au uwezo mkubwa zaidi, na mchango wao wa hadhara kwa kanisa unaweza kuonekana kuwa mkubwa zaidi. Kufuatia mafanikio yao makubwa kiuchumi, baadhi yao wanaweza kutoa zaidi ya wengine. Katika hali ya namna hiyo, kuna kawaida ya asili ya kibinadamu ya kuwathamini watu fulani zaidi kuliko tunavyofanya kwa wengine. Walakini hali kama hiyo si sahihi machoni pa Mungu. Tunaweza kufikiri juu ya mifano miwili; mjane maskini aliyetoa sarafu mbili tu ndogo, bado Yesu alimsifu na akasema kwamba alitoa zaidi ya wengine wote. Katika Yakobo 2, Yakobo analaumu kitendo cha kuonesha upendeleo au kutoa heshima zaidi kwa matajiri wanaoweza kuingia katika makusanyiko yetu. Mungu anawachukulia wakristo wote sawa katika thamani, pasipo kuangalia tofauti zozote za nje zinazoweza kuwepo katika jamii zetu, nasi tunapaswa kufanya hivyo.

Zaidi ya hayo, katika 1Wakorintho 12 Paulo analinganisha kanisa na mwili wa binadamu. Kama vile mwili ulivyo na viungo vingi tofauti tofauti, kila kimoja na kazi tofauti, ndivyo ilivyo katika kanisa, kuna washirika wengi na kila mmoja ana kazi yake. Hata hivyo mshirika aliyedhaifu asichukuliwe kama yeye si wa muhimu, bali kila mmoja afanye kazi kwa ajili ya umoja na ujenzi wa mwili mzima. Katika mwili wa binadamu, hata kama kiungo kimoja tu hakifanyi kazi sawa sawa, hatuuchukulii ule mwili kuwa ni mkamilifu na wenye afya. Kadhalika, kanisa ambalo washirika hawajaungana wote na hawana usawa katika thamani, lisichukuliwe kuwa ni kanisa lenye afya.

Kanuni hiyo hiyo inaweza kuonekana katika uhusiano baina ya makusanyiko. Mara nyingi kazi ya kusanyiko moja inafanyika pasipo kufikiria madhara yanayoweza kusababishwa katika kazi nyingine au katika makusanyiko mengine. Mara nyingi makanisa yanafanya ushindani, kila moja likitaka liwe kubwa zaidi. Wakati hakuna ubaya wowote kufanya jitihada za kukua, inatupasa kuyafikiria makusanyiko mengine. Ukristo si kama mashindano katika biashara, ambapo biashara ndogo zinaondolewa na biashara kubwa, na wakati wengine huenda wakahuzunishwa na hali hiyo, tunaichukulia hali hiyo kama ni ya asili tena ni ya kawaida. Makanisa yanapaswa kutumia rasilimali zao kuyasaidia mengine badala ya kuzitunza kwa ajili ya

matumizi yao tu. Haiwezi kutokea kamwe kuona mazingira ambayo mshirika mmoja wa Uungu anajifanyia jambo lake mwenyewe bila kujali madhara juu ya washirika wengine. Kwa hiyo, tunapochukua picha ya Uungu, makusanyiko yanatakiwa kujali ustawi wa makusanyiko mengine.

Kanuni hiyo hiyo inaweza kuonekana hata katika familia zetu. Hakuna mshirika (mwana familia) anayetakiwa kuwa si wa muhimu au hana thamani katika familia husika. Kadhalika hakuna mtu anayetakiwa kuwa mvivu au kuchangia kidogo kwenye ustawi wa nyumba (familia). Katika Uungu wote wameshikamana na wanafanya kazi kwa lengo moja; kwa hiyo, tunapochukua taswira ya Mungu katika maisha yetu, ndipo kila mmoja nyumbani anafanya kazi kwa ushirikiano kwa manufaa ya familia, badala ya kila mmoja kibinafsi kujitafutia kwa tamaa zake mwenyewe.

## Hitimisho

Tumekuwa tukijadili tofauti ambazo Uungu unafanya katika maisha yetu. Mungu na Kristo wanaishi katika maisha ya watumishi wao. Paulo anaandika katika Wagalatia 2:21 **nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu…** Kama Mungu anaishi ndani yetu, basi tunapaswa kuelewa asili yake. Tunapojadili mara kwa

mara namna sisi kama wakristo tunavyotakiwa kuwa na uhusiano kila mmoja na mwenzake, mara nyingi tunasahau au hatujui hasa ni kwa nini. Kwa kawaida tunasema kirahisi kuwa upendo unatutaka tutende kwa namna fulani. Hilo ni kweli, lakini hata hivyo bado tunarudi kwa Mungu, kwa kuwa Mungu ni upendo (1Yohana 4:8). Kwa vyovyote vile tunavyotendeana katika hali yoyote, hatimaye tunarudi katika umoja na upendo uliothibitika katika Uungu. Tukiondoa Uungu tutakuwa tumeondoa msingi ule ambao katika huo tunaona kielelezo cha maisha yetu. Je, hapo tunaona tofauti yoyote? Natumai utakubali kwamba ipo tofauti kubwa.

## Maswali ya kujipima

1. Uungu unarejea kwenye nini?

2. Je, hali ya Yesu kuwa katika mwili inarejelea kitu gani?

3. Ni matokeo gani muhimu ya Mungu kuvaa mwili?

4. Ni kitu gani ambacho Yakobo analaumu katika Yak.2?

5. Kufikiria kuhusu Uungu kuna athali (matokeo) gani juu ya majukumu katika familia?

**Kweli/ Si kweli**

1. Dini zote zina fundisho linalofanana la Uungu.

   Kweli / si kweli.

2. Katika mawazo ya watu wengi, Uungu una umuhimu mdogo kihalisia.

   Kweli / si kweli

3. Wakristo wote wana thamani sawa kwa kila mmoja.

   Kweli / si kweli.

4. Makusanyiko yanatakiwa kujiangalia yenyewe na kuonesha kujali kidogo ustawi wa makusanyiko mengine.

   Kweli / si kweli

5. Uungu ni msingi ambao katika huo tunaona kielelezo cha maisha yetu.

   Kweli / si kweli

## 2

## YESU NI MUNGU

Wengi wanakubali kuwa Mungu Baba ni Mungu. Mtu yeyote amwaminiye Mungu anaamini kwamba Mungu Baba ni Mungu, kwa hiyo tutachukulia kuwa ni kweli. Swali tutakaloliwasilisha katika somo hili ni kwamba Yesu ni Mungu au lah!

### Kuwepo kwake kabla.

Aya moja inayothibitisha wazi uwepo wa Yesu kabla ya maisha yake ya duniani ni Yohana 1:1 "**hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa Mungu"**. Tunaona tofauti kati ya Neno na Mungu kwa sababu Neno alikuwa na Mungu. Ungekuwa ni ujinga kusema Mungu alikuwa na Yeye mwenyewe. Bado tunaona kwamba Neno alikuwa Mungu, yaani asili yake alikuwa Mungu. Tunaiona tofauti hiyo hiyo katika aya ya 14, tunaposoma kwamba Neno akafanyika mwili, jambo ambalo ni wazi kabisa hurejelea kwa Yesu. Yohana Mbatizaji anatangaza katika aya ya 15 kwamba Yesu alikuwa mkuu kuliko yeye, kwa sababu alikuwako kabla yake. Yesu aliishi kabla ya Yohana, lakini alizaliwa kimwili miezi sita baada ya Yohana.

Katika Yohana 8:58 Yesu alisema, **“ yeye Ibrahimu asijakuwako Mimi niko”**. Hayo maneno “Mimi niko” yalitumika katika Kutoka 3:14-15 kumaanisha uwepo wa Yehova Mungu. Yesu hakuwa anasema tu kwamba alikuwa hai kabla ya Ibrahimu au kwamba ni kupata mwili kwa mara nyingine kwa Ibrahimu, bali alihusisha namna ile ile ya Mungu Baba kujidhihirisha, anajiweka kuwa sawa na Mungu na kwamba yupo mwenyewe kama Mungu.

Yesu alikuja kutoka mbinguni. Katika Yohana 3:13 Yesu anazungumza na Nikodemo na kusema, **Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila Yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani Mwana wa Adamu**. Mwana wa Adamu ni wazi kuwa humrejelea Yesu Mwenyewe, hivyo, Yesu hudai kuwa alikuwa hai mbinguni kabla hajaja duniani. Yesu anatoa madai kama hayo katika Yohana 6:51, **Mimi ndimi chakula chenye uzima kishukacho kutoka mbinguni**. Zaidi ya hayo, Yesu anatangaza katika Yohana 6:62, **Itakuwaje basi mmwonapo Mwana wa Adamu akipaa huko alikokuwako kwanza?** baada ya kifo chake, Yesu alirejea mbinguni alikokuwako kabla hajaja duniani.

Wayahudi wote waliikubali **Zaburi** ya **110** kuwa ni Zaburi ya Kimasihi (imhusuyo Masihi). Katika aya ya kwanza tunasoma, **Neno la Bwana kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako**. Hii “Bwana” ya

kwanza ni Mungu Baba, na “Bwana” ya pili inarejea kwa Masihi. Kwa hiyo, Daudi, kwa uvuvio, anamwita uzao wake ambaye bado hajazaliwa “Bwana”. Je, ni kwa jinsi gani Masihi aliweza kuwa Bwana wake Daudi na pia uzao wake? Yesu anahusisha Zaburi hii kujirejelea Yeye mwenyewe**. …Imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana, akisema, Bwana alimwambia Bwana wangu, uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako kuwa chini ya miguu yako?” Basi Daudi akimwita Bwana, amekuwaje ni mwanawe? (Mathayo 22:43-45**). Hivyo, kama Yesu alikuwa Masihi, basi alistahili kuwepo kabla, au kwa maneno mengine ni Mungu. Wayahudi walikuwa na matatizo ya kulielewa hili kwa sababu ya uelewa wao mbaya juu ya Masihi.

## Majina Ya Mungu Yanatumika kwa Yesu.

Katika Isaya 42:8 Mungu anasema, **Mimi ni BWANA** {Yehova}; **ndilo jina langu**; **na utukufu wangu sitampa mwingine,..** Mathayo kwa uvuvio ananukuu Isaya 40:3, na kwa kufanya hivyo, jina “Yehova” linatumika kwa Yesu.

Katika Tito 2:13, Tito anatangaza kwamba tulitazamie tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na mwokozi wetu. Ona, Yesu anaitwa Mungu.

Labda tangazo la Uungu wa Yesu lililo wazi linapatikana katika Yohana 20. Yesu aliwatokea wanafunzi wake wote, isipokuwa Tomaso, na wanafunzi walipomwambia Tomaso kwamba wamemwona Yesu, alidai kwamba hawezi kuamini mpaka atakapoziona na kuzigusa alama za misumari katika mikono ya Yesu. Jumapili iliyofuata, Yesu akawatokea tena wanafunzi wake, safari hii na Tomaso alikuwepo. Baada ya kupata uthibitisho binafsi ya kwamba Yesu yu hai, Tomaso alisema, "**Bwana wangu na Mungu wangu"**. Neno lililo Mungu katika swala hili ni "Theos", ambalo limetumika mara nyingi katika Injili ya Yohana na daima linarejelea kwa Mungu. Kwa hiyo, tunalo tangazo thabiti ya kwamba Yesu ni Mungu kama ambavyo Mungu Baba ni Mungu.

Yesu anaitwa Alfa na Omega, yaani mwanzo na mwisho. Alfa ni herufi ya kwanza ya alfabeti za Kiyunani (Kigiriki), na Omega ni herufi ya mwisho ya alfabeti za Kiyunani. Yehova anatangaza katika Isaya 44:6, **Mimi ni wa kwanza na mimi ni wa mwisho, zaidi yangu mimi hapana Mungu**. Katika Ufunuo 1:8 tunasoma kwamba Mungu mwenyezi ni Alfa na Omega. Aya chache tu baadaye (1:17), Yesu anamwambia mtume Yohana kwamba Yeye ni wa kwanza na wa mwisho. Vyeo hivyo hivyo vinatumika kwa wote wawili Yesu na Mungu mwenyezi, kuthibitisha kwamba hawa wawili wako sawa.

Katika Waebrania 5:9 tunasoma kuwa Yesu ni mwanzilishi au chanzo cha wokovu kwa wote wamtiio. Hakuna wokovu katika jina lingine (Matendo 4:12). Hakuna mwingine ila Mungu anayeweza kuwaokoa wanadamu kutoka katika dhambi zao. Yusufu aliambiwa katika Mathayo 1:21 kumwita mtoto jina Yesu, kwa sababu angewaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao. Kwa kuwa Kristo anafanya yale ambayo ni Mungu pekee ndiye awezaye kuyafanya, hiyo inamaanisha Yesu ni sawa na Mungu. Pia Yesu, aliitwa Imanueli, likiwa na maana Mungu pamoja nasi.

Paulo anatangaza katika Wakolosai 2:9 kwamba ukamilifu wa Mungu unakaa ndani ya Yesu, lakini sio Mungu Mwenyewe. Paulo anaposema Ukamilifu wa Mungu unakaa ndani ya Yesu, anamaana kwamba kila kitu kinachomkamilisha Mungu kuwa Mungu, pia hukaa ndani ya Yesu. Kwa maneno mengine, Yesu ni Mungu maadamu Baba ni Mungu.

### Sifa muhimu za Mungu Anapewa Yesu.

Yesu ni wa milele kama vile Mungu. Isaya aliandika katika Isaya 9:6, **"maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa mabegani mwake; Naye ataitwa jina lake, mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani".** Majina yote haya ni majina ya Mungu katika sehemu nyingine

za maandiko. Waebrania 1:8 ni nukuu kutoka Zaburi 45:6: **Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele.** Zaburi ya 45 ni wazi inarejea kwa Mungu, na Mwana ni mkuu kuliko malaika; kwa hiyo, tuna uthibitisho mwingine wa Uungu wa Yesu, kwa sababu aliumba vitu vyote (Wakolosai 1:16-17).

Yesu anatangazwa kuwa ni mwenye nguvu zote (omnipotent). Katika Yohana 1:3, Yohana anatangaza kwamba Neno aliumba vitu vyote. Aliyeumba vitu vyote ni Mungu (Waebrania 3:4); hivyo, kwa kuwa Yesu aliumba vitu vyote, bilashaka ni Mungu. Zaidi ya hapo, Paulo anatangaza katika Wakolosai 1:16, **Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana….vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake**. Yesu aliumba vitu vyote, kwa hiyo, bila shaka Yesu ni Mungu.

Yesu alijua mambo yote. Yohana anaandika katika Yohana 2:24,25, **lakini Yesu hakujiaminisha kwao; kwa kuwa Yeye aliwajua wote; na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu; kwa maana Yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu.** Ni wazi kuwa Mungu pekee ndiye anayeweza kujua mioyo ya wanadamu; kwa hiyo Yesu anatangazwa kuwa ni Mungu.

**Kazi za kiungu zilizoelekezwa kwa Yesu.**

Katika Yohana 6, baada ya kuwalisha watu 5,000, alisena Yeye ni chakula cha uzima (Yohana 6:48,51,53-58). Hii humaanisha kwamba Yesu kama chakula cha kiroho hukidhi uzima wa kiroho. Hakuna mtu wa kawaida ambaye angeweza kutoa madai haya. Katika Yohana 11:25-26 Yesu alisema Yeye ni ufufuo na uzima, halafu akamfufua Lazaro kutoka kwa wafu kuthibitisha madai hayo. Hii pia inaweza kuwa na maana kwamba ana uwezo wa kutoa uzima. **Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwahuisha, vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao** (Yohana 5:21). Kwa kuwa ni Mungu pekeyake anayeweza kuhuisha, basi bilashaka Yesu pia ni Mungu. Yesu alidai kuwa ni Bwana wa Sabato (Mathayo12:8). Kwa kuwa Mungu aliifanya Sabato, basi ni Mungu pekee angeweza kuwa Bwana wa Sabato.

Yesu alidai kuwa sawa na Mungu katika maeneo kadhaa. Alisema "**Mimi na Baba tu umoja"** (Yohana 10:30). Kwa usemi huo alikuwa na maana kuwa alistahili heshima sawa na Mungu. Wayahudi walielewa vizuri madai haya, kwa sababu waliokota mawe ili wamwue. Yesu alipokuwa akihojiwa, kuhani mkuu alimwuliza wazi wazi ikiwa "Yeye ni Kristo, Mwana wa Mungu" (Mathayo 26:63-64). Katika kiapo, Yesu alisema, "Mimi ndiye'. Alidai kuwa na nguvu za kusamehe dhambi, na kila mmoja alijua kuwa ni Mungu

pekee aliye na uwezo wa kusamehe dhambi. Katika Marko 2:1-12 alimponya mtu aliyepooza baada ya kumwambia kuwa dhambi zake zimesamehewa. Ni Mungu peke yake angeweza kumponya yule mtu; kwa hivo, muujiza ulithibitisha madai ya Yesu. Pia Yesu alidai kuwa Yeye ni mhukumu wa watu wote. **Tena Baba hamhukumu mtu yeyote, bali amempa Mwana hukumu yote (Yohana 5:22).**

## Ibada ya Kimungu ilielekezwa kwa Yesu.

Katika Yohana sura ya 9 Yesu alimponya mtu aliyezaliwa kipofu. Baadaye kidogo, Yesu alizungumza na yule mtu na kumuuliza kama anamwamini Mwana wa Mungu, yule mtu akauliza mwana wa Mungu ni nani ndipo Yesu akajibu kwamba Yeye ndiye Mwana wa Mungu, angalia jibu la yule mtu, "**Naamini, Bwana. Akamsujudia"** (Yohana 9:38). Habari kama hiyo ilitokea katika Mathayo 14:33, **Nao waliokuwemo ndani ya chombo** {wanafunzi} **wakamsujudia, wakisema, hakika wewe u Mwana wa Mungu**. Yesu alikubali kusujudiwa, ambapo Myahudi halisi kwamwe asingeweza kufanya hivyo. Wayahudi wote walielewa kwamba Mungu peke yake ndiye aliestahili kuabudiwa. Yesu asingekubali kuabudiwa, na wanafunzi wake wasingemwabudu pasipo Yeye kuwa Mungu.

Tunasoma hata habari ya Mungu kuwaamuru malaika wamwabudu Mwanawe. Angalia Waebrania 1:6 **Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu**. Aya hii imenukuliwa kutoka Kumbukumbu La Torati 32:43. Mzaliwa wa kwanza kwa asili hurejelea Mwana wa Mungu au Yesu. Kamwe Mungu asingewaamuru malaika kumwabudu yeyote ambaye sio Mungu.

## Hitimisho

Kuna rejea nyingine nyingi ambazo zinaweza kutajwa zikionesha ama katika hali ambayo si ya moja kwa moja au moja kwa moja kwa Yesu kuwa ni sawa na Mungu, lakini hizi zilizotajwa zinatosha. Mtu ye yote aliyefunguka akili ambaye anaiamini Biblia anapaswa kuelewa kuwa Yesu ni Mungu kama vile Mungu Baba alivyo Mungu.

## Maswali ya kujipima

1. Usemi huu “Mimi Niko” unaonesha nini?

2. Je, ni kwa jinsi gani Masihi wa Zaburi 110 kuwa Bwana wa Daudi na uzao wake?

3. Ni nani aliyemtamka Yesu, “Bwana wangu na Mungu wangu”?

4. Pale Yesu alipotangaza kwamba Mwana wa Mungu huleta uzima, je, ni kwa jinsi gani hilo huthibitisha Uungu wake?

5. Yesu alikuwa na maana gani aliposema Mimi na Baba tu umoja?

**Kweli / si kweli**

1. Yesu alipodai kuwa aliishi kabla ya Ibrahimu, alikuwa anasema kwamba Yeye alikuwako kama Mungu alivyokuweko.

   Kweli / si kweli

2. Kwa kuwa Yesu ni Muumbaji, pia ni lazima awe Mungu.

   Kweli / si kweli

3. Kwa kuwa vyeo vile vile vinatumika kwa wote wawili, kwa Mungu na kwa Yesu, tunajua Yesu pia ni Mungu.

   Kweli / si kweli

4. Hakuna aliyemwabudu Yesu alipokuwa duniani.

   Kweli / si kweli

5. Yesu alidai kuwa Yeye ni mhukumu wa watu wote

   Kweli / si kweli

# 3

## ROHO MTAKATIFU NI MUNGU

Katika somo lililopita nilijadili juu ya ushahidi unaonesha kwamba Yesu ni Mungu, na sasa nitafanya hivyo hivyo juu ya Roho Mtakatifu. Somo hili ni gumu zaidi ya somo kuhusu Yesu. Ni vigumu zaidi kuitambua kazi Yake, na kumekuwa na matumizi mabaya ya kuhusiana na kazi Yake. Watu wengi wanazitazama zama hizi kama zama za Roho Mtakatifu; kwa hiyo, mara nyingi Roho huinuliwa hata zaidi ya Yesu na Mungu Baba. Kwa kweli, hayo yamekuwa matumizi mabaya ya fundisho la Biblia kuhusiana na Roho.

### **Roho Mtakatifu ni Nafsi**.

Roho Mtakatifu ana sifa za msingi za hali ya kuwa nafsi (Yohana 14:26; 15:26; 16:13-14). Katika vifungu hivi Yesu anamrejelea Roho Mtakatifu mara tisa kama nafsi. Ananena na anawapa wengine uwezo wa kunena. **Basi Roho anena wazi wazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani,..** (1 Timotheo 4:1).

Roho Mtakatifu hufundisha. **Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na**

**kuwakumbusha yote niliyowaambia** (Yohana 14:26). Roho Mtakatifu huongoza. **Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote…** (Yohana 16:13).

Roho Mtakatifu ana nia. **Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu.** (Warumi 8:27).

Roho Mtakatifu anamapenzi. **Ndugu zangu, nawasihi kwa Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa upendo wa Roho, jitahidini pamoja nami katika maombi yenu kwa ajili yangu mbele za Mungu** (Warumi 15:30).

Roho Mtakatifu ana matakwa. **Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, Yeye yule akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo Yeye** (1 wakorintho 12:11).

Roho Mtakatifu anaweza kuhuzunishwa. **Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi** (Waefeso 4:30).

## Roho Mtakatifu ni Mungu.

Moja ya matangazo yaliyo wazi sana ya Uungu wa Roho Mtakatifu linapatikana katika Matendo 5: 3-4. Tunawaona Anania na Safira wakiuza mali fulani na kupeleka sehemu ya mali hiyo kwa Mitume ili kuwasaidia maskini. Hata hivyo, Walidandanya kwamba walitoa kiasi chote cha mauzo kanisani. Katika aya ya 3 tunamuona Petro anamwambia Anania, **Kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu…?** Halafu, mwishoni mwa aya ya 4 tunaona maelezo haya kutoka kwa Petro, **Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu.** Kwa uvuvio, Petro anaeleza kuwa uongo huo ulisemwa kwa Roho Mtakatifu na kwa Mungu. Hili linaweka usawa kati ya Roho na Mungu Baba.

Katika Kumbukumbu La Torati 32:12 tunaona kwamba Mungu peke yake aliwaongoza Israeli Jangwani; bado katika Isaya 63:10 tunasoma kwamba Israeli walimwasi na kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Sehemu hizi hazipingani; badala yake huonesha kuwa Roho ni Mungu pia. Mungu Baba, Yesu na Roho wote walihusika katika kuwaongoza Israeli. Hali kama hiyo inaweza kuonekana kati ya Isaya 40:13 na Warumi 11:34. Katika Isaya 40, Isaya anauliza ni nani aliyemfundisha au kumshauri Roho. Paulo alinukuu aya hii katika Warumi 11 na akaihusisha na Mungu Baba, tena akionesha kwamba hawa wawili wako sawa.

## Roho ana Sifa za Uungu

Katika Waebrania 9:14 Roho anazungumzwa kama Roho wa milele. Roho pia anasemekana kuwa yupo kila mahali. Katika 1Wakorintho 6:19, kuwa yupo kila mahali, Paulo anauliza, **Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe.** Roho anasemekana kukaa ndani ya moyo wa kila mkristo. Kwa kuwa wakristo wametawanyika kila mahali ulimwenguni, swala la Roho kukaa ndani ya kila mkristo haliwezi kuwa kweli, isipokuwa tu kama Roho ana sifa ya Uungu wa kuwa kila mahali kwa wakati mmoja. Daudi alitambua kuwa haiwezekani kumkimbia Roho Mtakatifu (Zaburi 139:7). Zaidi ya hayo, Roho anasemekana kuwa anajua kila kitu (omniscient). Angalia 1Wakorintho 2:10 **Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.** Roho anasemekana kuwa anajua mambo ya ndani ya Mungu; kwa hiyo, ni lazima na Yeye pia ni Mungu. Mika anatangaza kuwa alijaa nguvu kwa Roho ya Bwana (Mika 3:8).

## Roho Anatenda Kazi Za Mungu.

Roho anasemekana kwamba alishiriki katika Uumbaji. Mwandishi wa Zaburi aliandika katika Zaburi 33:6, Kwa neno la Bwana aliandika katika Zaburi 33:6, **Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyanyika, Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.** Pumzi ni rejea ya Roho. Usemi kama huo umetumika katika Zaburi 104:30, **Waipeleka roho yako, wanaumbwa, Nawe waufanya upya uso wa nchi**. Si kwamba Roho alishiriki katika Uumbaji wa dunia tu, bali pia anaitunza na kuifanya upya.

Yesu anatangaza, **Roho ndiyo itiayo uzima** (Yohana 6:63). Ni Mungu pekee aliye na uwezo wa kutoa uzima, na hapa tuna maneno ya Yesu yanayosema kwamba Roho hutoa uzima; hivyo bila shaka Roho ni Mungu. Katika 1 Petro 3:18, Petro anazungumzia mateso na kuinuliwa kwa Kristo. Anaeleza kwamba Yesu aliteswa kusudi mwanadamu aje kwa Mungu. Yesu aliuawa kimwili, lakini alihusishwa na Roho. Katika Warumi 8:11 Paulo anasema kuwa Roho alimfufua Yesu katika wafu, pia atatuhuisha na sisi.

Ushahidi mwingine wa Uungu wa Roho Mtakatifu ni Yesu kupata mwili. Katika vitabu vyote viwili yaani cha Mathayo na Luka, inatangazwa kuwa Yesu alizaliwa au alitungwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Mathayo 1:20, Luka 1:35). Mtu anakuwa mwana wa

yule aliyezaliwa naye; kwa hiyo, tungeweza kusema kwamba Yesu ni Mwana wa Roho Mtakatifu. Lakini Yesu pia ametajwa sehemu kadhaa wa kadha kuwa Mwana wa Mungu. Kwa hiyo, bila shaka Roho Mtakatifu pia ni Mungu. Huu pia ni uthibitisho wa fundisho la umoja wa Mungu, ambao tutaujadili katika somo linalofuata. Kama watatu hawa si mmoja, basi Yesu ana mababa wawili.

## Roho Mtakatifu Kama Kitu Cha Kuabudiwa.

Katika 2 Wakorintho 13:4 tunaona Roho Mtakatifu anatajwa kama sehemu ya Uungu uliotukuka, **Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote.** Itakuwa kufuru kuweka jina lingine lolote katika ule utawala wa watatu ila kwa Mungu. Maelezo yanayofanana na hayo yanapatikana katika Agizo Kuu la Yesu katika Mathayo 28:19, **Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.** Kubatiza katika jina la mtu fulani ni kitendo cha kuabudu (1 Wakorintho 1:13). Kwa hiyo, Roho kama ilivyo kwa Yesu, anapata heshima na ibada ile ile kama ilivyo kwa Mungu Baba.

## Hitimisho

Kutokana na mjadala uliopita, natumaini sasa mtu anaweza kuona kwamba Roho Mtakatifu anazungumzwa kama Mungu na ana sifa za Uungu kama walivyokuwa nazo Mungu Baba na Yesu. Kwa hiyo, Roho ni Mungu pia. Katika somo linalofuata, tutaangalia namna Watatu wanavyoweza kuwa mmoja.

## Maswali ya kujipima

1. Ni nani aliyewaongoza mitume katika kweli yote?

2. Anania na safira walimwambia uongo nani?

3. Miili yetu ni hekalu la_________________.

4. Kubatizwa kwa jina la mtu fulani ni kitendo cha_________________________________.

5. Usemi: “anajua yote” unamaanisha nini?

**Kweli / si kweli**

1. Roho Mtakatifu hajawahi kurejelewa kamwe kama nafsi.

   Kweli / si kweli

2. Roho Mtakatifu na Mungu wanawekwa katika hali ya usawa katika aya kadhaa.

   Kweli / si kweli

3. Yesu alisema kwamba Roho ndiyo itiayo uzima.

   Kweli / si kweli

4. Ingeweza kusemekana kwamba Yesu ni Mwana wa Roho Mtakatifu.

   Kweli / si kweli

5. Roho Mtakatifu hakufanya lolote katika uumbaji.

   Kweli / si kweli

4

## BWANA MUNGU WETU NI MMOJA

Wazo linalofuata katika somo letu ni mjadala juu ya uhusiano kati ya Mungu Baba, Yesu na Roho Mtakatifu. Katika mtazamo wa kwanza, mtu anaweza kusema hawa ni miungu watatu, hivyo, Ukristo ni imani ya miungu wengi. Wazo linguine ni lile la kuamini kwamba hao watatu ni udhihirisho wa kawaida wa Mungu mmoja katika hali tofauti tofauti. Kwa maneno mengine, kuna Mungu mmoja tu, lakini kwa wakati fulani anazungumziwa kama Mungu Baba, Yesu au Roho Mtakatifu. Yesu ni udhihirisho tu wa huyo Mungu mmoja, na wakati mwingine Mungu hujidhihirisha kama Roho. Hii huondoa mtanziko wa kuwa na miungu watatu, lakini tunakabiliana na tatizo la kuweka uwiano wa fundisho hili na fundisho la Biblia.

Fundisho la Uungu ni wazo gumu sana kulielewa. Kwa kweli siamini kwamba tunaweza kuuelewa Uungu kikamilifu, lakini hili lisitushangaze. Kuna mambo mengi kuhusu Mungu ambayo wanadamu hawawezi kufahamu kikamilifu. Kwa mfano, wanadamu hawawezi kufahamu wazo la umilele, kwa sababu kila kitu hapa duniani kina mwanzo na mwisho. Hata hivyo, kwa ufafanuzi, umilele haukuwa na mwanzo na hautakuwa na mwisho. Japo tunaweza kutoa vielelezo fulani

vinavyoweza kuwasaidia wengine, vielelezo hivyo vinapungukiwa ufafanuzi wa kweli juu ya umilele. Tungekuwa tunaelewa na kufahamu kikamilifu mambo yote kuhusu Mungu, basi asingekuwa Mungu tena. Pale tu tunapodhani tunamwelewa Mungu kikamilifu, tayari tunakuwa tumemweka Mungu katika hali ya sanamu, na hapo atakuwa si Mungu tena. Hatutaki kumwabudu mtu au kitu ambacho si chochote, pasipo kujali ukuu wake ni wa namna gani.

## **Jitihada Za Kutatua Ugumu Huu**.

Isilete mshangao kwamba wanadamu wametunga mafundisho kadhaa yanayoonekana kuleta ufumbuzi juu ya ugumu wa Uungu. Angalia machache kati ya mafundisho makuu.

Njia moja ya kupata ufumbuzi ni kuelezea upya Uungu wa Yesu. Wazo hili linafundisha kwamba Yesu hakuwa Mungu kwa hali yoyote ile wakati wa ujauzito au kuzaliwa kwake, lakini baadaye aliasiliwa na Mungu na kuinuliwa hata kufikia nafasi ya Uungu. Mtu anaweza kumzungumzia Yesu kama Mungu kwa sababu kwa uwezo mkubwa Mungu alikuwa anafanya kazi ndani yake na kupitia kwake wakati wa maisha yake hapa duniani. Hili linaondoa wasiwasi kati ya Uungu wa Yesu na Mungu; hata hivyo wazo hili linayakataa na kutoyaona maeneo mengi ya Biblia yanayofundisha

usawa kati ya Yesu na Mungu na Uungu wa Yesu tangu kutungwa mimba na hata kabla ya kutungwa mimba.

Mtazamo mwingine ni ule ambao tayari umekwisha kutajwa, unaomwonesha Mungu kama mhusika katika mchezo ambaye anachukuwa nafasi kadhaa katika mchezo; wakati mmoja Mungu anacheza katika nafasi ya Mungu Baba; mwingine anachukuwa nafasi ya Yesu; wakati mwingine anachukua nafasi ya Roho. Kwa hiyo, Mungu kwa kweli si nafsi tatu bali ni nafsi moja inayoonekana katika namna tatu tofauti. Wazo hili linalinda umoja wa Mungu; lakini hupuuza vifungu kadhaa vya maandiko ambavyo kwavyo tunaona wote watatu wapo kwa wakati mmoja. Yesu alipobatizwa, Mungu alizungumza kutoka mbinguni na Roho alishuka juu ya Yesu kama huwa (Luka 3: 21-22). Je, Yesu alipokuwa duniani alimwomba nani? Utakuwa upumbavu kusema Yesu alijiomba mwenyewe. Mungu alipokuwa kijusi (kitoto) tumboni mwa Mariamu, angewezaje kuidhibiti na kuitunza dunia? Hivi kiukweli Mungu angewezaje kuwekewa mipaka ya maarifa kama Yesu alivyowekewa alipokuwa duniani (mf. Marko 13:32), kama alikuwa mmoja na ni nafsi ile ile?

Ufumbuzi mwingine katika dini za ulimwenguni kuelezea upya uhusiano uliopo kati ya Baba na Mwana. Badala ya kushikilia kwamba Yesu ni wa milele, mtazamo huu humwelezea Yesu kama kiumbe tu, kiumbe cha kwanza tena chenye nafasi ya juu kuliko

viumbe vingine vyote, lakini hata hivyo, Yesu ni kiumbe kilichoumbwa na kwa hivyo, ni wa hali ya chini (mdogo) kuliko Mungu. Vifungu kadhaa vya Agano Jipya vinaonekana kuunga mkono wazo hili. Kwa mfano, Yesu alisema,**…Baba ni mkuu kuliko mimi** (Yohana 14:28). Katika Marko 10:18 na hata Luka 18:19, Yesu alijitofautisha na Mungu aliposema, **… kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, naye ndiye Mungu**. Lakini, kama ilivyo kwenye hoja nyingine, mtazamo huu huzipuuza vifungu vingi vinavyofundisha uwezo na asili ya milele ya Yesu ambayo ilielezwa katika somo la 2. Vifungu vya Agano Jipya vinavyoelezea ukuu wa Baba dhidi ya Mwanawe vinaweza kueleweka kama ni namna ya kuonesha kujishusha kwa hiari kwa Yesu katika sifa za Uungu kama inavyooneshwa katika Wafilipi 2:5-11 alipofanyika mwili.

## Mungu ni Mmoja.

Fundisho hili linafundishwa katika Biblia nzima. Wayahudi, mara kwa mara walinukuu Kumbukumbu La Torati 6:4, wakiita Shema (shema ni jina la mmoja wa watu waliosimama mkono wa kuume wa Ezra iliposomwa Torati), **Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja.** Yesu pia alinukuu aya hii katika Marko 12:29. Amri ya kwanza katika Amri kumi inasema, **usiwe na miungu mingine ila Mimi**. Isaya alionya dhidi ya ibada za sanamu katika

matukio mengi; angalia mifano miwili tu. **… Mimi ni wa kwanza na Mimi ni wa mwisho; zaidi yangu Mimi hapana Mungu** (Isaya 44:6). Usemi unaofanana na huo unatolewa katika sura inayofuata. **Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu Mimi hapana Mungu;…**(Isaya 45:5). Paulo alitoa maelezo yanayofanana na hayo katika 1 Wakorintho 8:4, **… hakuna Mungu ila mmoja tu.** Tunajifunza kutoka katika Yakobo 2:19 kwamba hata mashetani wanaamini kuna Mungu mmoja tu.

Je, watatu wanawezaje kuwa mmoja? Hilo ni tatizo ambalo sisi wanadamu tunalo. Hatuwezi kufikiria habari ya vitu vitatu vilivyo tofauti kuunganishwa kuwa kitu kimoja na bado vikabakia kuwa vitu vitatu vilivyo tofauti. Katika somo linalofuata tutaangalia zaidi juu ya wazo hili la Mungu kuwa mmoja, na pia kufikiria baadhi ya milinganisho ambayo inaweza kutusaidia vema kuelewa wazo hili gumu.

## Maswali ya kujipima

1. Taja mambo mawili katika somo hili yaliyotajwa ambayo hatuwezi kuyaelewa kikamilifu.

2. Tunajuaje kuwa Mungu sio mhusika (mwigizaji) tu akijionesha katika namna tatu tofauti tofauti?

3. Kwa nini Yesu akiwa katika mwili alionekana mdogo kuliko Mungu?

4. Wayahudi waliitaja Kumbukumbu La Torati 6:4?

5. Yakobo alisema kuna miungu wangapi?

**Kweli / si kweli**

1. Ibada si jambo (wazo) gumu sana kulielewa.
   Kweli / si kweli

2. Tunaweza kuelewa kikamilifu wazo La Mungu.
   Kweli / si kweli

3. Njia moja ya kawaida ya kutatua hoja ya Uungu ni kuamini kwamba Yesu alikuwa kiumbe wa kwanza.
   Kweli / si kweli

4. Mashetani yanaamini kuwepo kwa miungu wengi.
   Kweli / si kweli

5. Amri ya kwanza katika Amri kumi inasema kwamba tusiwe na miungu mingine ila Mungu wa kweli.

   Kweli / si kweli

5

## NINI MAANA YA NAFSI TATU KATIKA UMOJA?

Tumeona kwamba Mungu ni mjumuisho wa Nafsi tatu, ambazo kila moja ina sifa zote za Uungu. Biblia inaonesha Nafsi tatu, na tatu tu, wakiwa na vyeo vya Kiungu. Angalia Hagai 2:5-7. **Kama neno lile nililoagana nanyi mlipotoka katika nchi ya Misri; na roho yangu inakaa kati yenu; msiogope. Kwa maana BWANA wa majeshi asema hivi, mara moja tena, ni kitambo kidogo tu, nami nitazitikisa hizo mbingu, na hii nchi, na bahari, na nchi kavu; nami nitatikisa mataifa yote, na vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote vitakuja; nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema BWANA wa majeshi.** Hao watatu wanatajwa kama Mungu: Bwana wa Majeshi, Roho, na vitu vinavyotamaniwa na Mataifa Yote. Vitu vinavyotamaniwa na Mataifa Yote ni wazi vinamrejea Yesu. Katika hali ya namna hiyo, hao watatu wanatajwa kama Mungu na kumetajwa pamoja katika Mathayo 28:19, **Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.** Katika sehemu hii ya maandiko, neno “jina” liko katika umoja. Kwa hivyo, hao watatu wanaunda jina Moja. Zaidi ya hayo, mtume

Paulo anarejea kwa wote watatu katika 2 Wakorintho 13:14. **Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote.**

Wazo la Uungu lisingetegemewa kuonekana sana katika Agano la kale, lakini bado taarifa nyingi katika Agano la kale kwa hakika zinakubaliana na fundisho la Uungu. Moja ya mambo yaliyo wazi ni matumizi ya wingi katika kuliheshimu jina la Mungu. Ikiwa Mungu ni mmoja, basi mfumo wa umoja tu ulipaswa utumike kwa kumheshimu Mungu. Hata hivyo, jina la Mungu kwa Kiebrania, Elohim lipo katika wingi. Si lazima kwa hilo jina tu basi imaanishe kuwa Mungu ametajwa katika wingi, lakini angalia katika Mwanzo 1:26. **Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu…**Neno "akasema" lipo katika umoja, lakini kitenzi "tumfanye" kiko katika wingi, kama ilivyo "kwa sura yetu" na "kwa mfano wetu". Mifano mingine inayofanana na huo inaweza kupatikana: **BWANA mungu akasema, "Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya;…"** Mwanzo 3:22. Angalia mfano mwingine tena, sasa hivi ni katika Isaya 6:8. Kisha nikasikia sauti ya Bwana, akisema, **"Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"** Kubadilika kwa hesabu kutoka umoja kwenda wingi ni kwa muhimu sana

## Tunawezaje Kuelewa Uungu?

Tumeona kwamba Biblia wazi wazi inatangaza kuwa Mungu ni mmoja, lakini wakati huo huo inatangaza na kuonesha wingi katika muundo katika maeneo mengine. Tunawezaje kuelewa dhana hii ya siri? Mungu ni Mmoja, lakini si mmoja katika idadi, ila mmoja katika asili ya umoja. Fikiria kifungu kilicho bora kabisa cha umoja katika Biblia, Kumbukumbu La Torati 6:4-5 **Sikiza, Ee Israeli, BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja.** Kiebrania kina maneno mawili kwa ajili ya neno "Moja". Neno la kwanza linaonesha "moja" au "upekee", kama vile Ibrahimu alivyoambiwa amtoe mwanawe wa pekee. Neno linguine, ambalo limetumika katika Kumbukumbu La Totati 6 linaonesha "Umoja" au "Vitu kadhaa kwa pamoja". Neno hili hili limetumika katioka Mwanzo 2:24, **kwa hiyo Mwanaume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.**

Milinganisho mingi imependekezwa ili kuelezea Uungu lakini hakuna hata mmoja ulio kamili. Uungu umefananishwa na maji, ambayo yanaweza kuwepo katika hali ya Yabisi, kimiminika au mvuke. Tatizo kubwa la kielelezo hicho ni kwamba maji hayawezi kuwa katika hali zote tatu, kwa wakati mmoja. Uungu umefananishwa na yai ambalo lina ganda, kiini na ute mweupe lakini bado ni yai moja. Uungu pia

umefananishwa na vitu kadhaa vya kimwili. Kielelezo kingine ni kama vile mwanadamu anavyoweza kuwa baba, mwana na mume, hali zote kwa wakati mmoja. Tatizo la kielelezo hiki ni kwamba mtu mmoja hawezi kuwa baba, mwana na mume kwa wakati mmoja. Mimi binafsi napenda kielelezo kutoka katika Biblia. Kwenye Mwanzo 1, Mungu ameamuru kuwa mtu awaache baba na mama na kuambatana na mkewe, na watakuwa mwili mmoja. Kiukweli wanabakia watu wawili waliotengana, lakini wanakuwa wameungana kikamilifu. Kama kilivyo kielelezo hicho, katika Yohana 17:11 Yesu aliomba kuwa wakristo wawe na umoja kama vile Yeye na Mungu walivyo na umoja. Ni dhahiri wakristo wote katika hali halisi hawazezi kuwa mtu mmoja. Hali kadhalika, Paulo alisema kwamba, “Yeye apandaye na yeye atiaye maji ni wamoja”. Kwa hakika, tunapaswa kutambua kwamba vitu vinayozuia umoja kwa wanadamu, haviwezi kuzuia kwa Mungu. Kwa hiyo, Uungu umeshikamana kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko wa wanadamu.

Njia nyingine ya kuutazama Uungu ni kuangalia Uungu kama jamii, nafsi tatu. Wamefungamanishwa pamoja na upendo kwa kuwa Mungu ni upendo (1 Yohana 4:8,16). Upendo unawafungamanisha pamoja kwa karibu sana kiasi kwamba wao ni wamoja. Upendo unahitaji kuwepo mtu anayesikiliza (anayeongozwa) na mtu anayepaswa kusikilizwa. Kwa hivyo, kabla ya

Uumbaji, Mungu asingeweza kupenda kama hakuwa zaidi ya mmoja. Hili linaweza kuonekana halitoshi, lakini kuna mambo kadhaa kwa wanadamu ambayo hayapo kwa Mungu. Tumetenganishwa na miili ya nyama. Kwa kuwa Mungu ni roho, yeye hana mipaka. Wanadamu wote wanatofautiana katika uzoefu wa maisha ambao unaathiri namna zote za maisha yetu. Ni dhahiri kwamba shida hiyo nayo haipo kwa Mungu. Wanadamu wote wanatingwa kila mmoja kwa sehemu yake, mahitaji na matatizo ya mtu binafsi, lakini hali hiyo ya kutingwa si sehemu ya asili ya Mungu. Mambo haya yote, labda na mengine zaidi, yanafanya isiwezekane kwetu kutazama na kuelewa au kuwa na uwezo wa kutambua kikamilifu na kusisitiza kwa wanadamu wengine; lakini mipaka yote hiyo haiko hivyo kwa Mingu, kwa hiyo, Yeye anaweza kuunganishwa kikamilifu kwa kiwango cha juu zaidi kuliko jinsi ilivyo kwa wanadamu.

## Hitimisho

Katika mfululizo huu wa masomo tumekuwa tukijaribu kuelezea wazo la Uungu. Tukiwa hatuwezi kuelewa kikamilifu jambo hili, kwa matumaini somo hili limetuwezesha kuufahamu zaidi Uungu huo, na zaidi ya hayo, limetuimarisha imani zetu juu ya fundisho hili Muhimu sana. Uungu umeundwa na nafsi tatu au vituo

vitatu vya ufahamu, lakini nafsi zote zimeshikamana kikamilifu kiasi kwamba zimekuwa moja. Nafsi zote tatu katika Uungu zimeingiliana kila moja na nyingine. Kila nafsi hutoa uhai kwa nyingine, na zote zinahusika katika hali zote za kazi ya Mungu.

## Maswali ya kujipima

1. Ni wangapi wameongelewa katka Biblia wenye nyadhifa za Uungu?

2. Isaya anawaitaje hawa watatu?

3. Mungu ni mmoja katika_________au_________

4. Kipi kinaunganisha Uungu pamoja?

5. Ni sifa zipi za wanadamu ambazo huzuia umoja wetu kuwa kama ule alionao Mungu?